JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU

*(Mawasiliano yote yafanyike kupitia kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali)*

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na.: AC 334/376/01/382** **Tarehe: 08 Septemba, 2026**

# YALIYOJITOKEZA

# FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI AGOSTI, 2026

## 1. MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

### 1.1 Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa (FBT) ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Kapu linalotumika kukokotoa FBT lina jumla ya bidhaa 383 ambazo bidhaa 132 ni za Vyakula na Vinywaji Baridi, na bidhaa 251 ni bidhaa zisizo za vyakula. Kwa wigo wa kijiografia, FBT zinakokotolewa kwa kutumia takwimu za bei zinazokusanywa kwenye makao makuu ya mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

### 1.2 Mizania za Fahirisi na Kizio

Mizania za Fahirisi za Bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa maeneo ya mijini na vijijini. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18 yalitumika kama chanzo kikuu cha takwimu za uandaaji wa mizania za Fahirisi. Kizio cha Bei cha Fahirisi zilizofanyiwa marejeo kimeboreshwa na kuwa wastani wa bei za mwezi Januari hadi Disemba 2020, na kizio cha Fahirisi ni mwaka 2020.

### 1.3 Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa zinatumia mpangilio wa kimataifa wa matumizi binafsi ujulikanao kama COICOP "*Classification of Individual Consumption by Purpose*" wa mwaka 2018. Aidha, Fahirisi za Bei zinatolewa kwenye makundi 13 ya mpangilio wa COICOP, 2018 pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu ambayo yanajumuisha: - Fahirisi za msingi (*core index*); Fahirisi ya nishati, mafuta na huduma za maji; Fahirisi isiyo ya msingi *(Noncore index);* Fahirisi ya huduma; Fahirisi ya bidhaa; Fahirisi ya huduma za elimu na bidhaa zinazoambatana nazo na Fahirisi ya bidhaa zote isiyojumuisha bidhaa za vyakula na vinywaji baridi.

### 1.4 Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi za mwanzo unatumia wastani wa jiometria "*geometric mean of Price Relatives*". Kanuni ya Fahirisi ya *Lowe Index Formula* ambayo ni aina ya "*Laspeyres Index Formula*" hutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Takwimu House, 64 Barabara ya Lusinde, S. L. P. 2683,
41104 Tambukareli – Dodoma, Tanzania. Simu: +255 26 – 2963822 Barua pepe: sg@nbs.go.tz;
Tovuti: www.nbs.go.tz

## 2 MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KWA MWEZI AGOSTI, 2026 UMEFIKA ASILIMIA 4.3

**Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Agosti, 2026, (2020 = 100)**

| Na. | MAKUNDI MAKUU YA FAHIRISI | Mizania (Weight) | Agosti., 2025 | Julai., 2026 | Agosti., 2026 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 130.48 | 135.79 | 135.36 | -0.3 | 3.7 |
| 2 | Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 112.90 | 114.67 | 114.62 | 0.0 | 1.5 |
| 3 | Mavazi na Viatu | 10.8 | 114.77 | 116.69 | 116.89 | 0.2 | 1.8 |
| 4 | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | 15.1 | 118.10 | 120.73 | 121.08 | 0.3 | 2.5 |
| 5 | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 116.32 | 118.90 | 119.39 | 0.4 | 2.6 |
| 6 | Afya | 2.5 | 109.55 | 111.12 | 111.14 | 0.0 | 1.5 |
| 7 | Usafiri | 14.1 | 119.69 | 136.11 | 136.18 | 0.1 | 13.8 |
| 8 | Habari na Mawasiliano | 5.4 | 106.32 | 106.90 | 107.88 | 0.9 | 1.5 |
| 9 | Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 111.19 | 111.72 | 111.98 | 0.2 | 0.7 |
| 10 | Huduma za Elimu | 2.0 | 111.99 | 115.29 | 115.55 | 0.2 | 3.2 |
| 11 | Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 117.29 | 120.51 | 120.79 | 0.2 | 3.0 |
| 12 | Huduma za Bima na Fedha | 2.1 | 102.36 | 102.60 | 102.58 | 0.0 | 0.2 |
| 13 | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 118.36 | 122.21 | 122.26 | 0.0 | 3.3 |
| | **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | **100.0** | **119.77** | **124.85** | **124.93** | **0.1** | **4.3** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Fahirisi za Msingi (*Core Index*) | 73.9 | 115.98 | 120.44 | 120.74 | 0.3 | 4.1 |
| 2 | Fahirisi Isiyojumuisha Fahirisi za Msingi (*Non-Core Index*) | 26.1 | 130.51 | 137.38 | 136.83 | -0.4 | 4.8 |
| 3 | Fahirisi za Nishati, Mafuta na Bili za Maji | 5.7 | 130.72 | 141.76 | 141.85 | 0.1 | 8.5 |
| 4 | Fahirisi za Huduma | 37.2 | 112.69 | 119.16 | 119.34 | 0.2 | 5.9 |
| 5 | Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 123.96 | 128.22 | 128.24 | 0.0 | 3.5 |
| 6 | Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 114.32 | 116.24 | 116.42 | 0.2 | 1.8 |
| 7 | Bidhaa zote isipokuwa bidhaa za chakula na bidhaa za vinywaji visivyo na kilevi | 71.8 | 115.56 | 120.56 | 120.84 | 0.2 | 4.6 |

### 2.1 Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa Kipimo cha Mwaka

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026 umeongezeka hadi asilimia 4.3 kutoka asilimia 4.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2026. Ongezeko hili linaashiria kuwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma katika mwaka ulioishia Agosti 2026 ilikuwa kubwa zaidi ikilinganishwa na kasi iliyorekodiwa katika mwaka ulioishia Julai 2026. Fahirisi za Bei zimeongezeka kutoka 119.77 mwezi Agosti, 2025 hadi 124.93 mwezi Agosti, 2026, ikionesha ongezeko la jumla la bei za bidhaa na huduma katika kipindi hicho.


### 2.2 Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026 umepungua hadi asilimia 3.7 kutoka asilimia 4.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2026. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei ambao haujumuishi Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Agosti, 2026 umeongezeka hadi asilimia 4.6 kutoka asilimia 4.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2026.

## 2.3 Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (Core Inflation)

Fahirisi za bei za msingi zinaandaliwa kwa kutojumuisha bidhaa za vyakula zisizochakatwa; nishati na bili za maji. Kutojumuisha bei za bidhaa ambazo zina sifa ya kubadilika mara kwa mara kwenye Fahirisi za bidhaa na huduma zote, hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera. Fahirisi za bei za msingi zinakokotolewa kwa kutumia bei za bidhaa na huduma 297 na mchango wa mizania kwenye Fahirisi zote ni asilimia 73.9. Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (*Core inflation*) kwa mwezi Agosti, 2026 umeongezeka hadi asilimia 4.1 kutoka asilimia 3.9 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2026.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Agosti, 2025 hadi Agosti, 2026. (2020 = 100)**




Kielelezo Na. 1 kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwelekeo wa ongezeko kwa ujumla kati ya mwezi Agosti 2025 na Agosti 2026, zikiongezeka kutoka 119.77 hadi 124.93. Katika kipindi hicho, Kiwango cha Mfumuko wa Bei kiliendelea kuwa katika kiwango cha wastani, kikiwa kati ya asilimia 3.2 na asilimia 4.3. Kiwango hicho kilipungua hadi asilimia 3.2 mwezi Februari na Machi 2026, kabla ya kuongezeka hadi asilimia 4.0 mwezi Aprili, kufikia asilimia 4.2 mwezi Mei, kushuka hadi asilimia 4.0 mwezi Juni, na kuongezeka tena hadi asilimia 4.2 mwezi Julai na asilimia 4.3 mwezi Agosti 2026.

## 3 FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KATI YA MWEZI JULAI 2026 NA AGOSTI, 2026

Fahirisi za Bei za Taifa kati ya mwezi Julai, 2026 na Agosti, 2026 zimeongezeka kutoka 124.85 hadi 124.93. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: mchele kwa asilimia 1.9; unga wa ngano kwa asilimia 0.7; vyakula jamii ya tambi kwa asilimia 0.5; kuku hai kwa asilimia 4.2; nyama ya ngombe kwa asilimia 0.6; nyama ya kuku kwa asilimia 0.6; samaki wabichi kwa asilimia 2.3; dagaa wakavu kwa asilimia 1.4; mayai ya kuku kwa asilimia 2.2; mafuta ya kupikia chakula kwa asilimia 0.9; karanga mbichi kwa asilimia 2.4; viazi vitamu kwa asilimia 0.2; sukari kwa asilimia 0.5; juisi za viwandani kwa asilimia 0.8 na vinywaji visivyo na kilevi kama soda na vinywaji vya kuongeza nguvu (*energy drinks*) kwa asilimia 0.2. Kwa upande mwingine baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: vitambaa vya kushona nguo kwa asilimia 1.4; nguo za wanaume, wanawake na watoto kwa asilimia 0.2; viatu vya wanaume kwa asilimia 0.1; bidhaa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa jengo kama saruji na mabati kwa asilimia 1.9; gesi kwa matumizi ya kaya kwa asilimia 0.4; kuni kwa asilimia 1.3; mkaa kwa asilimia 1.7; samani za nyumba kama; sofa, vitanda, viti na kabati za nguo kwa asilimia 0.4; bidhaa kwa ajili ya usafi wa nyumba kama kama sabuni ya kufulia nguo kwa asilimia 2.3; bidhaa na huduma kwa ajili ya michezo, starehe na utamaduni kwa asilimia 0.2; huduma ya chakula, vinywaji visivyo na kilevi na vinywaji vyenye kilevi kwa asilimia 0.2 na bidhaa na huduma kwa ajili ya usafi binafsi kwa asilimia 1.4.

**Jedwali Namba 3: Ratiba ya Utangazaji Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo.**

| Fahirisi za Bei za Taifa | Tarehe ya Toleo |
|---|---|
| Septemba, 2026 | 08 Oktoba, 2026 |
| Oktoba, 2026 | 09 Novemba, 2026 |
| Novemba, 2026 | 08 Desemba, 2026 |